



TAARIFA ZA HAKA KUHUSU

Machaguo ya Bima ya NY State of Health Wakati wa Dharura ya Virusi vya Korona

Unastahili huduma ya afya ya bei nafuu.

NY State of Health ni bima rasmi ya afya ya New York Marketplace.

Jiandikishe leo.



Mtandaoni katika nystateofhealth.ny.gov



Kwa simu kupitia
1-855-355-5777
TTY: 1-800-662-1220



Ungana na Msaidizi wa Usajili kwenye info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho na za jimbo zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsi, umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

NY State of Health ipo hapa kwa ajili yako. Tunajitolea kukusaidia kupata bima unayohitaji ili upate huduma unayohitaji.

Ikiwa Huna Bima:

- Yeyote asiye na bima ya afya anapaswa **kutuma ombi sasa** kupitia NY State of Health.
- New York ilifungua kipindi cha usajili maalum cha “hali za kipekee” kwa yeyote ambaye hana bima kutuma ombi la bima ya Qualified Health Plan.
- Usajili uko wazi kwa Mipango yote ya NY State of Health. Medicaid, Essential Plan, Child Health Plus na Qualified Health Plans.

Ikiwa Umepoteza Kazi na Bima yako ya Afya:

- Ikiwa umepoteza bima ya afya ya mwajiri wako, **tuma ombi sasa** kupitia NY State of Health.
- Huenda ukastahiki kwa bima bila malipo au ya bei nafuu kupitia Medicaid, Essential Plan, Child Health Plus, au unaweza kustahiki Qualified Health Plan pamoja na miamana ya ushuru.
- Wasiliana nasi, tembelea tovuti yetu au zungumza na msaidizi wa usajili ili upate maelezo zaidi.
- Tuma ombi kupitia Marketplace ndani ya siku 60 baada ya kupoteza bima ya afya ya mwajiri.

TAARIFA ZA
HARAKA KUHUSU

Machaguo ya Bima ya NY State of Health Wakati wa Dharura ya Virusi vya Korona

Ikiwa Una Bima kupitia NY State of Health lakini Hali Zako Zimebadilika:

- Yeyote ambaye ameshuhudia mabadiliko katika mapato, ajira, au tukio jingine kubwa katika maisha, anaweza kustahiki kwa usaidizi zaidi wa fedha unaoweza kupunguza gharama zako. Sasisha taarifa ya akaunti yako leo- mtandaoni au kwa kuwasiliana na msaidizi wa usajili.
- Wasajiliwa wote wa Medicaid, Child Health Plus, au Essential Plan ambao wanahitajika kulipia bima Aprili au Mei 2020 tarehe zao za kulipa zitaongezwa kwa miezi minne.
- Watu binafsi waliojisajili katika bima iliyoruzukiwa au isiyoruzukiwa katika Jimbo la New York wanaweza kuwa na muda zaidi wa kulipa ada zozote za bima wanazodaiwa kipindi cha dharura ya afya ya umma. Taarifa zaidi kuhusu vipindi hivi ya nyongeza ya kulipa inapatikana kupitia [Department of Financial Services](#) na [NY State of Health](#).

Kuna Njia Tatu za Kutuma Ombi:

1: Jisajili Kupitia Tovuti Yetu: nystateofhealth.ny.gov

- Tutembelee mtandaoni na uturuhusu tukusaidie kupata bima ya huduma ya afya inayokufaa.

2: Jisajili kwa Simu kupitia kwa Msaidizi wa Usajili

- Maelfu ya wasaidizi wa usajili wako tayari kwenye jimbo zima kusaidia. Bofya kimoja cha viungo hapa chini ili umpate:
 - [Pata kipengele cha Kusogeza hapa](#)
 - [Pata Wasaidizi wengine wa Usajili hapa](#)

3: Jisajili kwa Simu kupitia Huduma kwa Wateja: 1-855-355-5777

Taarifa za ziada kuhusu Virusi Vipya vya Korona [zinapatikana hapa.](#)
Rudi tena ili uendelee kupata taarifa.